

Mungu Anakupenda!



MUNGU ALITUUMBA, DUNIA YETU NA VYOTE VILIVYOMO

Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.

—Mwanzo 1:1

BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa kiumbe hai.

—Mwanzo 2:7

Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au milki, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake.

—Wakolosai 1:16

Jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake.

—Zaburi 100:3a


Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila kiumbe kitambaacho nchini. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.

—Mwanzo 1:26-27

Mungu aliumba mwanadamu ili aishi naye milele.

The Scriptures used are from "BIBLIA, MAANDIKO MATAKATIFU, Swahili Union Version" © Bible Society of Kenya, © Bible Society of Tanzania, 1997.

"Mungu Anakupenda!" kitabu cha kupaka rangi Hati miliki © 2023 na World Missionary Press, Inc.



MUNGU AKAWAWEKA ADAMU NA HAWA KATIKA BUSTANI YA EDENI

BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, “Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, lakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.” —Mwanzo 2:15-17

***Nyoka, ambaye alitwa ibilisi au Shetani,
alileta mashaka kuhusu mamlaka ya
Mungu, na kusema uongo***

Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa.

Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alichuma matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala. —Mwanzo 3:4, 6

***Shetani ni adui wa mioyo yetu. Pia ni baba wa
mwongo. Tusimsikilize kamwe***

Yeye [Shetani] alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa uongo. —Yohana 8:44b



KUTOMTII MUNGU KULILETA DHAMBI NA KIFO KWA MWANADAMU

BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi?

Akasema, Nilisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha.

Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?

Adamu akasema, Huyu mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.

BWANA Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya?

Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala.

—Mwanzo 3:9-13

Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.

—Warumi 5:12

Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

—Warumi 3:23

Tangu siku ile mpaka sasa, kila mtu amezaliwa na asili ya dhambi moyoni mwake, siku moja atakufa kwa sababu kifo kililetwa na dhambi.



MUNGU ALIMTUMA MWANAWE KUTUOKOA

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipo-tee, bali awe na uzima wa milele. —Yohana 3:16

Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu. Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyoandikwa hapo Kirenio alipokuwa mtawala wa Shamu. Watu wote wakaenda kuandikwa, kila mtu mjini kwao. Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Yudea mpaka katika mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa ukoo na jamaa ya Daudi; ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba. Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni. —Luka 2:1-7

Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye. —1 Yohana 4:9

Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto wa kiume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani. —Isaya 9:6

Kuingia katika hali ya ubinadamu, Mwana wa Mungu lazima aje kama mtoto mchanga.



WACHUNGAJI NA MAMAJUSI WA MASHARIKI WALIKARIBISHA KUZALIWA KWAKE YESU KRISTO

Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafla, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe.

Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.

Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha Bwana. Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini.

—Luka 2:8-16

Nao [mamajusi wa mashariki] walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno. Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu, uvumba na manemane.

—Mathayo 2:10-11

***Vilevile Yesu anaitwa Imanueli, yaani
“Mungu pamoja nasi.”***



KWELI YESU KRISTO NI MWANA WA MUNGU ALIYE HAI

Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara aliibuka kutoka majini na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, na kutua juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni Mwangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.

—Mathayo 3:16-17

Pia jina jingine la Yesu ni NENO

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.

—Yohana 1:1-4

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. —Yohana 1:14

Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.

—Waebrania 1:1-2

Yesu ni Mungu—Alikuwa katika mwili wa binadamu.



YESU HAKUSHINDWA NA MAJARIBU YA SHETANI

Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arubaini mchana na usiku, mwishowe akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ikiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate.

Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini; kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.


Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako.

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka katika mlima mrefu mno, akamwonesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukiinama na kunisujudia.

Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Mwabudu Bwana Mungu wako, na umtumikie yeye peke yake. Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia.

—Mathayo 4:1-11

***Yesu alitumia neno la Mungu
kushinda kila jaribu.***



MUNGU ALITUPA SHERIA YAKE ILI ITUFUNDISHE JINSI YA KUISHI

Usiwe na miungu mingine ila mimi.

Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia.

Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.

Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.

Usiue.

Usizini.

Usiibe.


Usimshuhudie jirani yako uongo.

Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alichonacho jirani yako. —Kutoka 20:3-4, 7-8, 12-17

Yesu alitupa amri mbili kuu

Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. —Mathayo 22:37-39

***Tunapotii sheria ya Mungu, tunaonyesha upendo
kwa Mungu na upendo kwa watu wote.***



YESU AWACHAGUA WASAIDIZI— “NJOONI, MNIFUATE”

Naye alipokuwa akipita kando ya bahari ya Galilaya, akamwona Simoni na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. Yesu akawambia, Njoooni mnifuate, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata.

Akaendelea mbele kidogo, akamwona Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, nao pia walikuwa katika mashua, wakizitengeneza nyavu zao. Mara akawaita, wakamwacha baba yao Zebedayo ndani ya mashua pamoja na wafanya kazi wakaenda, wakamfuata.

—Marko 1:16-20

Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri.

—Marko 3:13-14

Bali Yesu akawaita waje kwake, akasema, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao. —Luka 18:16

***Yesu bado anaendelea kutuita—
“Njoooni, mnifuate.”***




MOJA YA MAHUBIRI MAKUU YA YESU

Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri wenye huzuni; maana hao watafarijika. Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi. Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa. Heri wenye rehema; maana hao watapata rehema. Heri wenye moyo safi; maana hao watamwona Mungu. Heri wapatanishi; maana hao wataitwa wana wa Mungu. Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri ninyi watakapowashutumumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu. —Mathayo 5:3-12

Yesu pia alitufundisha jinsi ya kuomba

Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatumizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.] Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. —Mathayo 6:9-15



MIUJIZA MBALIMBALI AMBAYO YESU ALIIFANYA ALIPOKUWA DUNIANI

Yesu alimtakasa mwenye ukoma

Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa. Yesu akanyosha mkono, akamgusa, akisema Nataka; takasika. Na mara ukoma wake ukatakasika. —Mathayo 8:2-3


Yesu alituliza dhoruba

Kukawa na msukosuko mkuu baharini, hata mashua ikafunikwa na mawimbi; naye alikuwa amelala usingizi. Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe, tunaangamia. Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba? Mara akaondoka, akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu. —Mathayo 8:24-26

Yesu alilisha umati

Yupo hapa mtoto, ana mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa? Yesu akasema, Waketisheni watu. Na mahali pale palikuwa na majani tele. Basi wanaume wakaketi, wapata elfu tano jumla yao. Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka. Nao waliposhiba, aliwaambia wanafunzi wake, Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote. —Yohana 6:9-12

Wanafunzi walipoona miujiza ambayo Yesu alitenda, waliamini kuwa yeye ni Mwana wake Mungu.



YESU KRISTO ANA UWEZO WA KUSAMEHE DHAMBI

Yesu anasamehe dhambi za mtu aliyepooza kisha anamponya

Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne. Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo; na wakiisha kulivunja wakaliteremsha godoro alilolilalia yule mwenye kupooza.

Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako.

Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao, Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?

Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza), Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako. Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Hatujawahi kuona jambo kama hili kamwe. —Marko 2:3-12



YESU KRISTO ANA UWEZO JUU YA KIFO

Yesu alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu


Yesu akasema, Liondoeni jiwe. Martha, dada yake yule aliyefariki, akamwambia, Bwana, ananuka sasa; maana amekuwa maiti siku nne. Yesu akamwambia, Mimi sikukuambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu? Basi wakaliondoa lile jiwe. Yesu akainua macho yake juu, akasema, Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nilijua ya kuwa wewe wanisikia sikuzote; lakini kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nilisema haya, ili wapate kusadiki kwamba ndiwe uliyenituma. Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, akiwa amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake amefungwa lesu. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake. —Yohana 11:39-44

Yesu anamfufua mwana wa mjane kutoka kwa wafu

Na alipolikaribia lango la mji, hapo palikuwa na maiti anachukuliwa nje, ni mwana pekee wa mamaye ambaye ni mjane, na watu wengi mjini walikuwa pamoja naye. Akakaribia, akaligusa jeneza; wale waliokuwa wakili-chukua wakasimama. Akasema, Kijana, nakuambia, Inuka. Yule maiti akainuka, akaketi, akaanza kusema. Akampa mama yake. —Luka 7:12, 14-15

Yesu alisema, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima.

—Yohana 11:25a



YESU ALIYATOA MAISHA YAKE ILI KUTUOKOA KUTOKA DHAMBINI

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. —Warumi 6:23

Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. —1 Yohana 5:11


Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuwapo kinywani mwake. Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakutisha; bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki. Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti. —1 Petro 2:22-24a

Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae tena. Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe. Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao na uweza wa kuutwaa tena. Agizo hilo nililipokea kwa Baba yangu. —Yohana 10:17-18

Amwaminiye Mwana ana uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia. —Yohana 3:36

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. —Yohana 14:6

Kifo cha Yesu msalabani kilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu wa kutupa uzima wa milele pamoja naye.



אֵלֶּיךָ חָצוּרָה יְמֵלֶךְ הַיְיָ
IHSVS NAZARENVS DEI FILIVS
IHSVS NAZARENVS DEI FILIVS

YESU ALIFUFUKA KUTOKA KWA WAFU

Na sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi. Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la ardhi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akalivingirisha lile jiwe akalikalialia. —Mathayo 28:1-2

Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, Msio-gope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa. Hayupo hapa; maana amefufuka kama alivyosema. Njoooni, mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia.

Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari.

Na tazama, Yesu akakutana nao, akisema, Salamu! Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia. Kisha Yesu akawaambia, Msio-gope; nendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakoniona.

—Mathayo 28:5-10

Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja wali-pokuwa wakila, akawakemea kwa kutoamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu. —Marko 16:14

Yesu alisema, Kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai. —Yohana 14:19b



JINSI YA KUMPOKEA YESU AWE MWOKOZI WAKO

Kusikitika kweli kwa dhambi zako (tubu)

Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. —Warumi 3:23

Ziungame dhambi zako kwa Yesu

Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote. —1 Yohana 1:9

Ziache dhambi zako

Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema. —Mithali 28:13

Mwamini Kristo awe Mwokozi wako


...Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka.
—Matendo 16:31a

Mpokee moyoni mwako

Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.
—Yohana 1:12

Mwongozo wa Maombi

Mpendwa Bwana Yesu,
Asante kwa kufa msalabani ili kuchukua dhambi zangu. Samahani kwa mambo yote mabaya ambayo nimefanya. Ninakuomba tafadhali unisamehe dhambi zangu, ingia moyoni mwangu na uishi moyoni mwangu milele. Ninakuamini sasa hivi kuufanya moyo wangu kuwa safi. Ninakuchukua kuwa Bwana na mwokozi wangu mwenyewe. Asante kwa kunifanya kuwa mtoto wako.
Kwa jina lako naomba amina.



MAMBO YA KUKUSAIDIA KUMFUATA YESU KWA UAMINIFU

Soma Neno la Mungu, Biblia takatifu, kila siku

Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu. —Zaburi 119:105

Kufafanuliwa kwa maneno yako kunatia nuru, na kumfahamisha mjinga. —Zaburi 119:130

Omba wakati wo wote mchana na usiku

Jioni, asubuhi, na aduhuri nitalalama na kuugua, naye ataisikia sauti yangu. —Zaburi 55:17

Mtumaini Bwana kila siku

Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.

—Mithali 3:5-6

Onyesha upendo kwa watu wote

Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama Mungu katika Kristo alivyo-wasamehe ninyi. —Waefeso 4:32

Endelea kutembea katika nuru aliyokupa Mungu

Bali tukienenda katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. —1 Yohana 1:7

Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima. —Yohana 8:12



KUZUNGUMZA NA MUNGU KWA MAOMBI

Ahadi za Mungu ziko kwa wamwombao

Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukio-mba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tunapoomba chochote, tunajua kwamba tumetimiziwa zile haja tulizomwomba.

—1 Yohana 5:14-15

Lazima kuomba kwa imani

Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.

—Marko 11:24

Tunapoomba ni lazima kwanza tusamehe

Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. [Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.]

—Marko 11:25-26

Ni vizuri kuomba na waumini wengine

Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.


—Mathayo 18:19-20

Kumtii Mungu kunaleta majibu ya maombi yetu

Na lolote tuombalo, tunalipokea kwake, kwa kuwa tunazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake.

—1 Yohana 3:22

Maombi ni kuwa na mazungumzo ya moyo kwa moyo na Mungu na kumruhusu Mungu pia kuzungumza na mioyo yetu.



ROHO WA MUNGU HUTUPATIA KARAMA ZA KUTUMIA KATIKA KUMTUMIKIA

Basi kuna karama tofauti; bali Roho ni yeye yule. Tena kuna huduma tofauti, na Bwana ni yeye yule.

—1 Wakorintho 12:4-5

Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.

—Waefeso 4:11-12

Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa; ikiwa ni unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani; ikiwa ni huduma, tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha, katika kufundisha kwake; mwenye kuonya, katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; msimamizi, na asimamie kwa bidii; anayerehemu, na arehemu kwa furaha.

—Warumi 12:4-8

Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo.

—Wakolosai 3:23-24

***Sio waamini wote wana karama sawa, lakini
Mungu humpa kila mwamini zawadi.***



UPENDO NDIO KARAMA KUBWA ZAIDI

Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliadini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.

—1 Yohana 4:16

Kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.

—Warumi 5:5b

Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi.

—Yohana 15:12

Karama zetu hazihesabiwi chochote, isipokuwa tuwe na upendo

Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, mimi si kitu. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidi kitu. Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. Upendo haupungui neno wakati wowote.

—1 Wakorintho 13:1-8a

Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya mata-tu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.

—1 Wakorintho 13:13



INAWEZEKANA BAADHI YETU WATATESWA KWA AJILI YA IMANU YETU KATIKA KRISTO

Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji la uzima. —Ufunuo 2:10

Kristo aliteswa kwa ajili yetu

Kwa sababu ndio mlioiwiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuata nyayo zake. Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuwapo kinywani mwake. Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakutisha; bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki. Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. —1 Petro 2:21-24

Kukariri mistari ya maandiko kutakupa nguvu

Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. —Zaburi 46:1-2

Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. —Yohana 16:33

***Huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu,
hiyo imani yetu. —1 Yohana 5:4b***



AMWAMINIYE YESU KRISTO, MCHUNGAJI MWEMA, ATAKUWA PAMOJA NAYE SIKU ZOTE

BWANA ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huniongoza. Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.

Naam, nijapopita kati ya bonde la kivuli cha mauti, Sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji.

Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele. —Zaburi 23

Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu. —Yohana 10:27-29

Sitakupungukia kamwe, wala sitakuacha. —Waebrania 13:5b

Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. —Mathayo 28:20b

***Wanaomfuata Yesu Kristo
watakuwa pamoja naye milele.***



ROHO MTAKATIFU WA MUNGU ANATUFUNDISHA NA KUTUBADILISHA TUNAPO SOMA NA KUTII NENO LA MUNGU

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki. —2 Timotheo 3:16

Jitahidi kujionesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mfanyakazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. —2 Timotheo 2:15

Heri wazitiio shuhuda zake, wamtafutao kwa moyo wote. Naam, hawakutenda ubatili, wamekwenda katika njia zake. —Zaburi 119:2-3

Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi. —Zaburi 119:11


Nitayatafakari maagizo yako, na kuziangalia njia zako. Nitajifurahisha sana kwa amri zako, Sitalisahau neno lako. —Zaburi 119:15-16

Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. —Warumi 12:2

Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema. —Wafilipi 2:13

Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. —Wafilipi 1:6

***Basi imani, hutokana na kusikia; na kusikia huja
kwa neno la Kristo. —Warumi 10:17***



YESU KRISTO, MWANA WA MUNGU, ANAKUJA TENA. UWE TAYARI!

Yesu aliahidi kwamba atakuja tena

Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo. —Yohana 14:1-3

Hakuna mtu ila Mungu anayejua ni lini Yesu atakuja tena

Lakini kuhusu siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake. —Mathayo 24:36


Yesu atakuja ghafla, kwa hiyo tunahitaji kuwa tayari

Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyaku-liwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. —1 Wathesalonike 4:16-17

Nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa saa msiyodhani ndipo ajapo Mwana wa Mtu. —Luka 12:40

Angalieni, kesheni, [ombeni], kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo. —Marko 13:33

Uwe tayari—Yesu yu karibu kuja!





MBINGUNI NI NYUMBANI KWA WALE WANAOMTUMAINI YESU

***Mbinguni ni mahali pazuri—
hakikisha umejiandaa kwenda kule***

Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio hali-kuyasikia, (Wala hayakuvingia katika moyo wa mwanadamu,) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.

—1 Wakorintho 2:9b

Mbinguni hakuna maombolezo, maumivu wala kifo

Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.

—Ufunuo 21:4

***Yesu hataki mtu yeyote ahukumiwe—Anataka tusaidie
kuwatayarisha wengine kwa ajili ya mbinguni***

Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa inakuja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.

—Yohana 5:28-29

Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nime-pewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, nendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabati-za kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

—Mathayo 28:18-20

Yesu Kristo ndiye njia pekee ya kwenda mbinguni!

Published in numerous languages by World Missionary Press, Inc., as God supplies funds in answer to prayer. **For questions or more information by country, visit: www.wmp-contacts.org**

Bure — Haipaswi kuuzwa



For enlarged coloring pages and other activities, visit www.wmpress.org/get-involved/kids-korner

World Missionary Press
PO Box 120
New Paris, IN 46553-0120 USA
www.wmpress.org 2-23



Read booklets online or by App
www.wmp-readonline.org

2803/2 Kiswahili GLY